

A Je; Neema inakuwaje nyingi ZAIDI dhambi inapozidi? Warumi 5:20.

- ❖ Neema ya Mungu inatosha kusamehe kila dhambi.
- ❖ Neema hutatua matokea mabaya ya dhambi.
- ❖ Neema hushinda kifo na kutupatia uzima wa milele katika Yesu.
- ❖ Neema inaweza kubadilisha.

B Kwa mujibu Warumi 6:1-11, wakristo hufia dhambi kwa njia ya ubatizo.

Hili linawezekanaje?

- ❖ Kupitia ubatizo...
 - Utu wetu wa kale unakufa (matamano yetu dhambi) na tunakuwa huru dhidi ya dhambi
 - Utu mpya unafufuka (hatuitumikii dhambi tena)
 - Tunaishi kwa ajili ya Mungu

C Utu wetu wa kale unakufa (matamano yetu dhambi) na tunakuwa huru dhidi ya dhambi. Utu mpya unafufuka (hatuitumikii dhambi tena) Tunaishi kwa ajili ya Mungu? Warumi 6:12.

- ❖ Utu wetu wa kale unakufa (matamano yetu dhambi) na tunakuwa huru dhidi ya dhambi
- ❖ Utu mpya unafufuka (hatuitumikii dhambi tena)
- ❖ Tunaishi kwa ajili ya Mungu.

D Je; 'Kutokuwa chini ya sheria, bali kuwa chini ya neema' huhusisha nini?

- ❖ 'kuwa chini ya sheria' humaanisha kutumia sheria kama njia ya kupata wokovu.
- ❖ Kuwa 'chini ya neema' humaanisha kutumia neema kama njia ya wokovu.

E Ikiwa hatuko tena chini ya sheria, kwa nini ni lazima tuitunze? Warumi 6:15.

- ❖ Kwa hiyo, inawezaje kuwa sawa au kuleta mantiki kusimama kwa hiari katika utumwa wa kwanza?
- ❖ Yeyote anayekataa kuongozwa katika utii wa sheria ya Mungu kwa neema yake ni kuikataa neema hiyo; anakataa uhuru na wokovu wa Mungu.

F Je; Wewe u mtumwa wa dhambi au wa utii? Warumi 6:16.

- ❖ Mtumwa wa dhambi = Mauti.
- ❖ Mtumwa wa utii = Haki.

G Tunawezaje kuwa watumwa wa utii? Warumi 6:18.

- ❖ Mafundisho sahihi hutusaidia kuwa "watumwa wa haki."

H Tunapata nini tunapowekwa huru dhidi ya dhambi? Warumi 6:19-23.

- ❖ Tunafanywa watumwa wa Mungu.
- ❖ Tunalo tunda letu la utakatifu.
- ❖ Tuna uzima wa milele katika Yesu, Bwana wetu.